

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA WAZIRI MKUU-SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA**  
**WALEMAVU**

Anwani ya simu: "KAZIAJIRA"

Simu Na: +255- (0)22 -2760548/2760552

Nukushi Na: (022) 2760552

Barua pepe: [info@osha.go.tz](mailto:info@osha.go.tz)

Mamlaka ya Usalama na Afya  
Mahali pa Kazi (OSHA),  
P.O Box 519,  
**DAR ES SALAAM.**



**Januari, 07, 2016**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**WITO KWA WAMILIKI WOTE WA SEHEMU ZA KAZI (WORKPLACES)  
KUSAJILI SEHEMU HIZO NA WAKALA WA USALAMA NA AFYA MAHALI PA  
KAZI (OSHA)**

Wakala inatambua kwamba kuna sehemu nyingi za kazi katika maeneo mbali mbali ya Tanzania Bara ambazo hazijasajiliwa jambo ambalo lilimsukuma **Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu-Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Walemavu, Mh. Jenista Mhagama** kutoa tamko rasmi kupitia vyombo vya habari lililowataka wamiliki wote wa sehemu za kazi kusajili sehemu hizo na Wakala ndani ya siku 14 tangu Desemba 14, 2015.

Kwamujibu wa kifungu cha 16 (1) cha Sheria ya Usalama na Afya ya mwaka 2003 (The Occupational Health and Safety Act, 2003), mmliki yeote wa kiwanda au sehemu ya kazi, anapaswa kuisajili na Wakala kabla ya kuanza kwa shughuli za uzalishaji katika kiwanda au sehemu ya kazi husika.

Kimsingi kusajili sehemu za kazi kunamwezesha Mkaguzi Mkuu (Chief Inspector) ambaye ndiye Mtendaji Mkuu wa Wakala kuzitambua sehemu zote za kazi na hivyo kuweza kupanga utaratibu wa kuzitembelea na kufanya ukaguzi ili kujiridhisha kama masuala yote yanayohusu Usalama na Afya Mahali Pa Kazi yanazingatiwa na hatimaye kutoa leseni za kukidhi viwango vya Usalama na Afya Mahali Pa Kazi.

Kwamujibu wa takwimu za usajili tulizokusanya katika kipindi hiki baada ya agizo la Mh. Waziri la Desemba 14, idadi ya sehemu za kazi zinazosajiliwa imeongezeka kwa zaidi ya mara mbili kwani awali tulikuwa tunasajili wastani wa sehemu za kazi sitini (60) kwa wiki na sasa zaidi ya sehemu za kazi mia moja hamsini (150) zinasajiliwa nchi nzima.

Pamoja na ukweli kwamba wamiliki wengi wameitikia wito wa Mh. Waziri kama takwimu zetu zinavyoonesha, lakini tunatambua kwamba idadi ya sehemu za kazi ambazo hazijasajiliwa na Wakala bado ni kubwa.

Hivyo tunawataka wamiliki ambao hawajatekeleza agizo la Mh. Waziri kuhakikisha kwamba wanatekeleza mara moja kabla hawajafikiwa na operesheni yetu ya kuwatambua inayoendelea nchi nzima.

Imetolewa na;

Dkt. Akwilina Kayumba

**Mtendaji Mkuu**

**Wakala wa Usalama na Afya Mahali Pa Kazi (OSHA)**